

MWONGOZO WA MAFUNZO YA MAANDALIZI YA MFUMO SHIRIKISHI WA UHAKIKI (PGS)

Umeandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) ulioandaliwa na TOAM kwa kushirikiana na wadau wa PGS Tanzania



MAANDALIZI YA MAARIFA HAYA

- Nakala hii ni tafsiri ya kiswahili ya mwongozo wa mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) uliotengenezwa awali kwa lugha ya Kiingereza kupitia ushirikiano wa shirika la kilimohai Tanzania (TOAM) na IFOAM – Organics International.
- Mwongozo huo ulishirikisha wadau wa PGS nchini Tanzania kuchangia ujuzi na maarifa ya namna mfumo huu unapaswa kutekelezwa.
- Kupitia mradi wa kitovu cha maarifa Afrika Mashariki (KHEA), TOAM iliweza kutafsiri mwongozo wa mafunzo haya kwa lugha ya Kiswahili ili kurahisisha matumizi yake kwa wadau mbali mbali wa mnyororo wa thamani. iliunga mkono tafsiri ya mwongozo huu kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili, kama sehemu ya kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa maarifa kuhusu PGS.

UTANGULIZI KUHUSU MAARIFA HAYA

- Mwongozo huu wa Mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) ni sehemu ya mfululizo wa nyenzo za mafunzo unaojumuisha moduli tano, zilizolenga kuwajengea washiriki uelewa na uwezo wa kutumia Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) katika Kilimohai.
- Nakala hii imejikita katika moduli 1 na inatoa maudhui kuhusu dhana za Kilimohai na Kilimoikolojia, uelewa wa mfumo ya uhakiki wa Kilimohai, PGS na historia ya PGS nchini Tanzania.
- Nakala nyingine za mafunzo kwa ajili ya moduli zinazofuata zinapatikana kama sehemu ya mfululizo huu, hivyo watumiaji wanashauriwa kuzitumia kwa pamoja ili kupata maudhui kamili ya mafunzo ya PGS.

MODULE YA KWANZA

UTANGULIZI WA DHANA ZA KILIMO IKOLOJIA HAI NA HISTORIA YA PGS

Kabla ya Kuanza Mafunzo:

1. Kujitambulisha
2. Kujadili Matarajio
3. Kujaza Fomu ya Tathmini Binafsi

Muhimu: Seti hii ya slides za mafunzo kwa moduli ya 1-5 inapaswa kutumika kwa kufuata mwongozo wa Mtaala wa Mafunzo ya PGS kwa Wawezeshaji (ToT), 2025

1.1 Utangulizi wa kanuni za kilimohai

Yaliyomo:

- Malengo ya kujifunza
- Kanuni nne za Kilimohai
- *Zoezi la 1: Mbinu zinazotumika kutekeleza kanuni za Kilimohai*



1.1 Utangulizi wa Kanuni za Kilimohai

Lengo la kujifunza:



Kuwawezesha washiriki kuelewa kanuni nne za Kilimohai na kuzitumia katika shughuli na utendaji ndani ya vikundi vyao vya PGS.

1.1 Utangulizi wa Kanuni za Kilimohai



Kanuni
ya Afya



Kanuni ya
Ikolojia




Kanuni ya
haki



Kanuni
ya kujali

Kanuni ya Afya



- Afya ni ukamilifu na uhai wa mifumo ya viumbe hai.
- Kilimohai kinapaswa kudumisha na kuboresha afya ya udongo, mimea, wanyama na sayari kama kitu kimoja kisicho tenganishwa

Kanuni ya Ikolojia

Kilimo Hai kinafanya kazi kwa kushirikiana na mazingira

Nafasi ya kuzingatia: Mfumo hai • Bioanuwai • Urejelezaji • Ustahimilivu

1. UDONGO NI MFUMO HAI



Udongo wenye afya, wenye viumbe hai huzaa mimea yenye afya.

2. BIOANUAI



Mazao mchanganyiko, miti, wanyama na wadudu rafiki hufanya mfumo kuwa imara na wenye tija.

3. UREJELEZAJI WA RASILIMALI



Tumia mboji, mabaki ya mazao na samadi kurejesha virutubisho udongoni.

MATOKEO YA KUILINGANISHA NA EKOLOJIA



Udongo wenye rutuba na hai



Mavuno bora na lishe bora



Matumizi bora ya rasilimali (kama maji na nishati)



Mazingira safi na usalama wa ikolojia



Maisha bora na ustahimilivu wa wakulima na jamii



4. USHIRIKIANO NA MAUMBILE



Tumia michakato ya asili kama udhibiti wa kiasi wa wadudu, utunzaji wa udongo na uhifadhi wa maji.

5. ULINZI WA MAZINGIRA



Hulinda maji, hewa, mazingira na viumbe hai kwa kupunguza uchafuzi na uharibifu.

6. USTAHIMILIVU NA ENDELEVU



Mfumo wa kilimo hai ni imara, hustahimili mabadiliko ya tabianchi na huleta tija kwa muda mrefu.

Kanuni ya Haki

Inasisitiza kujenga mahusiano yanayohakikisha:

- Upatikanaji sawa wa rasilimali na fursa
- Kukuza mazingira ya kazi yenye haki
- Wakulima wanapaswa kupata bei stahiki na malipo kwa wakati kwa mazao yao.
- Wanawake, wanaume na vijana wanapaswa kuwa na fursa sawa za kushiriki na kunufaika.



Kilimohai kinapaswa kujenga mahusiano yenye haki, heshima, uwazi na usawa kati ya watu wote wanaohusika katika mfumo wa chakula

Kanuni ya Kujali/ uangalizi

- Kilimohai kinapaswa kusimamiwa kwa tahadhari na uwajibikaji ili kulinda afya na ustawi wa kizazi cha sasa na kijacho pamoja na mazingira.
- Maamuzi ya uzalishaji yafanywe kwa kuzingatia athari zake kwa afya na mazingira
- Maamuzi ya leo yanapaswa kuimarisha uzalishaji na ustawi wa kesho

Fikiri kwanza kabla ya kutenda ili kulinda afya, mazingira na vizazi vijavyo.



Zoezi la 1: Jadili Mbinu za kilimohai ambazo zinatekeleza kanuni nne za Kilimohai

Majadiliano ya Zoezi la 2

Dakika 45



1.2 Utangulizi wa dhana ya Kilimoikolojia

Yaliyomo:

- Lengo la kujifunza
- Kanuni na vipengele 10 vya kilimoikolojia
- Zoezi la 2: Mbinu zinazotekeleza vipengele 10 vya Kilimoikolojia



1.2 Utangulizi kuhusu dhana ya Kilimoikolojia



Lengo la kujifunza

Kuwawezesha washiriki kuelewa dhana ya kilimoikolojia na vipengele vyake na kuweza kuvitumia katika shughuli za vikundi vyao vya PGS

Vipengele 10 vya kilimoikolojia

1. Anuai



2. Ushirikiano wenye matokeo ya ziada



3. Ufanisi



4. Ustahimilivu



5. Urejelezaji



6. Kushirikiana kuandaana kusambaza maarifa



Vipengele 10 vya kilimoikolojia

7. Maadili ya kibinadamu na Kijamii



9. Utawala unaowajibika



8. Mila na tamaduni za Chakula



10. Uchumi imara na uliofungamana



Tofauti kati ya Kilimohai na Kilimoikolojia

Kipengele	Kilimoikolojia	Kilimohai
Tafsiri ya dhana	Dhana pana na isiyo na ufafanuzi wa kina	Mfumo ulio tafsiriwa kwa kina
Viwango	Haina viwango rasmi vinavyotambulika na kutumika	Inaongozwa na viwango rasmi vinavyotambulika.
Uthibitishaji	Ni vigumu kuthibitisha kutokana na ukosefu wa viwango vilivyowekwa rasmi.	Inaweza kuthibitishwa kupitia mfumo wa uhakikisho kama vile PGS au uthibitishaji wa upande wa tatu (TPC)
Mada na tafsiri	Inaruhusu madai na tafsiri mbalimbali	Inatekelezwa kupitia viwango vilivyo wazi na vilivyothibitishwa
Vitu Vilivyo zuiliwa kutumiwa	Havijawekwa wazi na kufafanuliwa kikamilifu	Kuna zuio kali kuhusu matumizi ya viuatilifu vya kemikali, mbolea za viwandani na viumbe vilivyobadilishwa vinasaba

Zoezi la 2: Tambua mbinu za kawaida zinazotumika kutekeleza vipengele 10 vya Kilimoikolojia.



Majadiliano ya Zoezi la 3

Dakika 45

Maelekezo ya ziada: Katika vikundi, jadiliani na kuorodhesha mbinu zinazotekeleza vipengele vya kilimoikolojia katika jamii zenu



1.3 KUJENGA PGS KATIKA JAMII YAKO

KUELEKEA KUJENGA PGS KATIKA JAMII YAKO

Muhtasari:

- 1 Malengo ya kujifunza
- 2 Sifa za Mfumo wa uhakiki wa Kilimo Hai (OGS)
- 3 Kwa nini OGS ni muhimu?
- 4 Nani hutoa uhakiki wa ubora wa Kilimo Hai?
- 5 Tofauti kati ya aina tatu za OGS
- 6 Kwa nini uchague PGS?
- 7 Zoezi la 4 na 5



UAMINIFU



USHIRIKI



UWAJIBIKAJI



UENDELEVU



Lengo la kujifunza:

Kuwawezesha washiriki kuelewa dhana ya mfumo wa udhibiti ubora katika kilimohai.

Mfumo wa Uhakiki wa Kilimohai (OGS) ni utaratibu unaotumika kuthibitisha kuwa bidhaa za Kilimohai zinazalishwa kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa

Sifa za Mfumo wa Udhhibiti Ubora (OGS)

Mfumo wa Uhakiki wa Kilimohai (OGS) unajumuisha:

- **Kiwango cha Kilimohai:** Kiwango kinachoeleza mahitaji na kanuni ambazo wahusika wa mfumo ya kilimohai wanapaswa kuzingatia
- **Mfumo wa Uhakiki wa Ufuatiliaji:** Mfumo unaotumika kuthibitisha kuwa wahusika wanazingatia mahitaji ya kiwango husika.
- **Nembo ya Utambulisho wa Kilimohai:** Alama inayowekwa kwenye bidhaa zilizohakikiwa ili kuwasaidia walaji kuzitambua na kuzijengea uaminifu.

Kwa nini Mfumo wa Uhakiki ni Muhimu?

- Kujenga uaminifu kwa walaji wa bidhaa za Kilimohai
- Kuhakikisha kuwa bidhaa zinazouzwa kama za Kilimohai zinazingatia viwango vilivyowekwa.
- Kulinda wakulima na walaji dhidi ya udanganyifu katika soko la bidhaa za Kilimohai.
- Kukuza uwazi na uwajibikaji katika mfumo wa uzalishaji na biashara ya bidhaa za Kilimohai.

NANI HUTOA UHAKIKI WA KILIMOHAI?

Mhusika	Maelezo	Mfano
Mhusika wa kwanza	Mzalishaji mwenyewe hudai kuwa anazingatia viwango vya Kilimohai bila kuwa na uhakiki wa nje.	Mkulima kujitangaza kuwa anazalisha kwa kufuata kanuni za Kilimohai.
Mhusika wa pili	Uhakiki hutolewa na wadau wengine wanaohusika katika mnyororo wa thamani.	PGS ambapo wakulima, walaji, wanunuzi na wadau wengine hushiriki katika uhakiki.
Mhusika wa tatu	Uhakiki hutolewa na chombo huru cha uthibitishaji.	Uthibitishaji wa mtu wa tatu (TPC) wa Kilimohai unaofanywa na kampuni za uthibitishaji zilizoidhinishwa ili kukidhi viwango

Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) wa kilimohai

- Ni mfumo wa uhakiki wa ubora wa bidhaa za Kilimohai unaolenga masoko ya ndani.
- Hutoa uhakiki kwa **kushirikisha wadau** kama wakulima, walaji, wanunuzi na wawakilishi wengine.
- Unajengwa katika misingi ya **uaminifu, ushiriki, uwazi na kubadilishana maarifa.**

Kwa nini Uchague PGS?

- Huwawezesha hata wakulima wadogo kupata fursa za masoko ya bidhaa za Kilimohai.
- Huhakikisha uadilifu na ubora wa bidhaa za Kilimohai kupitia mfumo wa gharama nafuu na wenye uwazi.
- Huinua uchumi wa ndani kwa kuhamasisha uzalishaji na matumizi ya bidhaa za Kilimohai zinazozalishwa ndani ya jamii.



Zoezi la 4:

Jadili tofauti kati ya PGS na Uthibitishaji wa mhusika wa Tatu (TPC).

Zoezi la 5:

Jadili kufanana kati ya PGS na Uthibitishaji wa Mhusika wa Tatu (TPC).



Muda: Saa 1

TOFAUTI KATI YA PGS NA TPC

Kigezo	Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS)	Mfumo wa uhakiki na mhusika wa tatu (TPC)
Nyaraka	Huhitaji nyaraka chache	Huhitaji nyaraka nyingi na za kina
Uthibitisho	Hufanywa kwa kushirikisha wanakikundi na wadau wenza/wengine	Ukaguzi hufanywa na taasisi ya uthibitishaji
Uaminifu na ushiriki	Hutegemea ushiriki, uwazi na uaminifu wa wadau	Hutegemea uthibitisho wa taasisi huru
Uwazi	Kuwa na uwazi wa hali ya juu miongoni mwa wanachama	Inasisitiza usiri
Gharama	Nafuu kwa wakulima wadogo	Gharama kubwa zaidi
Soko Lengwa	Masoko ya ndani na ya kikanda	Masoko ya kitaifa na kimataifa
Mazao Yanayohakikiwa	Mazao yote ya shambani	Kwa kawaida, mazao mahususi yaliyoainishwa katika mfumo wa uthibitishaji
Chanzo cha viwango	Viwango vinavyotambulika na vilivyo tafsiriwa kulingana na mazingira ya eneo husika	Viwango vilivyowekwa na mamlaka za kimataifa za udhibiti

KUFANANA KATI YA PGS NA TPC

1	Zinazingatia zinazingatia kanuni za msingi za Kilimohai na kilimoikolojia
2	Zinaweza kutumika na wakulima wadogo.
3	Zinazingatia viwango vinavyotambulika vya Kilimohai.
4	Zinahitaji mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu na taratibu za usimamizi.
5	Huhakiki mfumo mzima wa uzalishaji wa shamba na haziruhusu uzalishaji sambamba wa mazao ya Kilimohai na yasiyo ya Kilimohai kwa zao moja.
6	Hutumia nembo au alama rasmi kutambulisha bidhaa zilizohakikiwa.


1.4 Historia ya PGS nchini Tanzania

Historia ya PGS Tanzania

Mahudhui

- PGS ilianzishwa Tanzania ili kuwezesha wakulima wadogo kupata uhakiki wa Kilimohai kwa gharama nafuu.
- Kikundi cha kwanza cha PGS kilikuwa Maendeleo Towelo, Morogoro.
- TOAM imekuwa na jukumu la kuratibu na kuendeleza PGS nchini.
- Alama ya Kilimohai Organic hutumika kutambulisha bidhaa zilizohakikiwa kwa kufuata viwango vya kilimohai Afrika Mashariki.

Ukuaji wa PGS Tanzania (2012–2026)



Idadi ya vikundi vya PGS nchini Tanzania imeongezeka kutoka kikundi 1 mwaka 2012 hadi zaidi ya vikundi 400 mwaka 2026.

Chanzo: Hifadhidata ya PGS ya TOAM, 2026.

Vikundi vya PGS Tanzania

Mkoa	Idadi ya Vikundi vya PGS
Morogoro	134
Mtwara & Lindi	172
Dodoma	45
Zanzibar (Unguja)	28
Njombe	10
Arusha & Moshi	10
Pwani	1
JUMLA	400

Vikundi hivi vya PGS vinajumuisha zaidi ya **wakulima 7,400** wanaolima takribani **hekari 16,000**. Mazao yanayozalishwa ni pamoja na viungo, matunda, mbogamboga, nafaka na jamii ya mikunde.

HITIMISHO

- Moduli hii imetoa utangulizi wa dhana muhimu za **Kilimohai, Kilimoikolojia na Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS)**. Pia imeangazia umuhimu wa mfumo wa uhakiki wa Kilimohai, tofauti na ufanano kati ya PGS na uthibitishaji wa mhusika wa tatu (TPC), pamoja na historia na maendeleo ya PGS nchini Tanzania.
- Katika Moduli ya 2 utajifunza zaidi kuhusu vipengele vinavyounda mfumo wa PGS na namna vinavyohusiana katika kuhakikisha uadilifu, uwazi, ushiriki na uaminifu katika mfumo wa uhakiki wa Kilimohai.

*Imeandaliwa na Shirika Mwamvuli la Kilimohai Tanzania
(TOAM) kupitia mradi wa kitovu cha maarifa Afrika Mashariki
(Knowledge Hub for Organic Agriculture and Agroecology
Tanzania - KHEA)*

Kupata moduli nyingine tembelea jukwaa la kidijitali la maarifa ya
kilimohai na kilimoikolojia katika tovuti: <https://khea-africa.org/>

Tunapatikana:

Mtaa wa Samora Avenue, Jengo la Kelvin House, gorofa ya Kwanza.
Kwa mawasiliano Zaidi tupigie kupitia +25574413499